



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI NJOMBE



08 Februari 2024.

TAARIFA KWA UMMA.

KAMPENI YA UTOAJI WA CHANJO YA SURUA NA RUBELLA.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe Bi.Kuruthum Sadick,anautaarifu umma kuwa ,kutakuwa na kampeni ya utoaji wa chanjo ya surua na rubella kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na wasiopungua miezi 9.

Chanjo hiyo itatolewa bila malipo kuanzia tarehe 15 hadi 18 Februari 2024 kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya ,ofisi za mitaa na vijiji,vituo vya kulelea watoto mchana (day care centers), kwenye maeneo ya mikusanyiko na shule zote za msingi zenye watoto wa darasa la awali.

Kumbuka chanjo hii itamkinga mtoto dhidi ya madhara yatokanayo na ugonjwa surua na rubella ikiwemo kifo au ulemavu wa kudumu.

Ewe mzazi/mlezi hakikisha mwanao anapata chanjo ya surua na rubella.

Imetolewa na:

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.

Ofisi ya Mkurugenzi (TD), S.L.P 577 NJOMBE, Tovuti: www.njombetc.go.tz, Simu: 026-2968833

Barua pepe: td@njombetc.go.tz, Posti Kodi : 31 Barabara ya Ikisa, 59108 Mjimwema -Njombe